MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.03: Msimu wa Kilimo 2026/27 *Tathmini ya Oktoba 21-31, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Novemba 1-10, 2026*

MUHTASARI


- Vipindi vya mvua vinavyotarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini na pwani ya kusini inaweza kusaidia ukuaji wa majani ya malisho kwa ajili ya mifugo, maandalizi ya mashamba na upandaji wa mazao kwa baadhi ya maeneo.
- Wakulima nchini wanashariwa kuendelea na maandalizi ya mashamba na kupanda mazao mara tu udongo unapokuwa na uynyevunyevu wa kutosha kuotesha mbegu
- Wadau wa kilimo wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kutoka TMA kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuendelea kubaki kusini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na bachi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi.

Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) lilikuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonesia). Hali hii iliimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi; na vipindi vya mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Oktoba 21-31, 2026

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2026

Katika dikadi hii, maeneo mengi ya mikoa ya Magharibi na kanda ya Ziwa Victoria na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi pamoja na nyanda za juu Kaskazini Mashariki yalipata kiasi cha mvua ya siku kumi cha kati ya milimita 1 hadi 100. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya Mara na Simiyu yalipata kiasi cha mvua cha zaidi ya milimita 100 kama inavyoonekana kwenye kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2026

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika baadhi ya maeneo nchini hususan maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na Pwani ya kaskazini zilisaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo, ukuaji wa majani kwa ajili ya malisho ya mifugo,maandalizi ya mashamba na upandaji wa mazao kwa baadhi ya maeneo ya .Wakati huohuo, baadhi ya maeneo hususan maeneo ya mikoa ya Mwanza na Musoma mazao tayari yalikuwa yamefikia hatua ya kuchipua.

Kwa upande wa mazao ya kudumu, zao la kahawa katika mkoa wa Moshi lilikuwa katika hatua ya uvunaji, zao la korosho katika mkoa wa Mtwara lilikuwa katika

hatua ya kukomaa, zao la karafuu katika wilaya ya Mheza mkoani Tanga lilikuwa katika hatua ya kukomaa. Halikadhalika, Kizimbani zao la karafuu lilikuwa katika hatua ya **'karafuu changa'**.

Kwa ujumla, upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo vimeendelea kuimarika katika baadhi ya maeneo kutokana na hali ya mvua iliyopo.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2026

Kwa ujumla, kina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya mito kilianza kuongezeka hususan katika baadhi ya maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2026

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukanda mvua kuendelea kubaki kusini, na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na maeneo machache ya kati ya nyanda za juu kusini magharibi.

Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonecia). Hali hii inatarajiwa kuimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi na yale yaliyoko nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2026

Maeneo kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kusini-magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) kunatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika baadhi ya maeneo hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma, maeneo ya kusini mwa Morogoro) na Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) kunatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa katika a maeneo mengi nchini inaweza kusaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo maandalizi ya mashamba , upandaji wa mazao kwa baadhi ya maeneo na ukuaji wa mazao katika maeneo machache hususan kanda ya Ziwa Victoria

USHAURI:

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini):** Wakulima wanashauriwa kupanda mazao mara tu udongo unapokuwa na unyevu wa kutosha kuotesha mbegu huku wakiendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (pwani ya kusini, maeneo ya magharibi, maeneo ya kati, nyanda za juu za kusini magharibi na maeneo ya kusini):** Wakulima wanashauriwa kuendelea na maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua unaokuja huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Wafugaji katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua** kwa mwaka wanashauriwa kupanda na kudumisha malisho ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha mifugo katika msimu huu wakati **wafugaji katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka** wanashariwa kuendelea kutumia maji na malisho ya mifugo yaliyopo kwa uangalifu. Aidha, wafugaji wote wanashauriwana kufuatilia kwa ukaribu utabiri wa hali ya hewa wa kila siku ili kufanya maamuzi sahihi na kupunguza hatari zinazohusiana na Hali ya Hewa.
- **Wavuvi wanaotumia Bahari na Maziwa makuu:** Wanashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku ili kuchukua tahadhari hususan wakati vinapojitokeza vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa majini.

Ushauri huu unalenga kuongeza tija ya kilimo na kupunguza athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kutumia taarifa za hali ya hewa kwa ufanisi na kushauriana na maafisa kilimo katika maeneo yao ili kufanya kilimo chenye tija.

HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mito kinatarajiwa kutofautiana kutokana na mtawanyiko wa mvua. Kuanza kwa mvua za Vuli kunatarajiwa kuongeza kina cha maji katika maeneo husika, huku ufuatiliaji wa mito na mabwawa ukiendelea kwa ukaribu kutokana na matarajio ya kuanza kwa msimu wa mvua.

Mkurugenzi Mkuu
S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)